Revial Ministries Australia

Inatoa

MISINGI

YA IMANI YETU

"Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na Imani kwa Mungu, na wa mafundisho ya mabatizo, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele".

Waebrania 6:1-2

Paul Galligan

YALIYOMO

SURA YA KWANZA **TUFANYE NINI TUPATE KUOKOKA?** 3
Tufanye nini tupate kuokoka?
Kujenga juu ya Mwamba.

SURA YA PILI **KUZITUBIA KAZI ZISIZO NA UHAI** 8
Kuzitubia kazi zisizo na uhai
Toba ikielekea kwa imani
Kuchimbua neno

SURA YA TATU **IMANI KWA MUNGU** 16
Imani kwa Mungu
Twaipokea aje imani?
Ibrahimu baba wa wote waaminio
Imani kwa Mungu kupitia Yesu Kristo

SURA YA NNE **FUNDISHO LA MABATIZO** 23
Fundisho la mabatizo
Ubatizo wa wakristo

SURA YA TANO **KUWEKEA MIKONO** 28
Mifano ya Agano la Kale
Mifano ya Agano Jipya

SURA YA SITA **KUFUFULIWA WAFU** 34
Kufufuliwa wafu
Kufufuliwa kwa Yesu Kristo
Kufufuliwa kiroho kwa waami
Kufufuliwa kwa mwisho kwa kila mtu aliyekufa

SURA YA SABA **HUKUMU YA MILELE** 41
Hukumu ya milele

SURA YA NANE **KUUFIKILIA UTIMILIFU** 48
Kuufikilia utimilifu
Kuweza kufundisha
Tunafundisha nini?

Nakala hii ya mafundisho ya mtu imetengenezwa ya mtu binafsi na pia ya kikundi.
Yote ni maandiko kuona kwamba misingi ya imani yetu imewekwa vyema.
Soma maandiko yote na ujaze mistari iliyowekwa.

NIFANYE NINI NIPATE KUOKOLEWA

Ile siku ya pentekosti katika **Matendo 2**, Petro alihubiri kuhusu kuja kwa Roho Mtakatifu na akapatiana ufahamu wa kushawishi wa kifo na kufufuka na kutukuzwa kwa Yesu**, aya 37** yasema: "***walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu***?". Jawabu ambayo petro alipeana pamoja na mambo mengine ambayo alikuwa amehubiri yanadhihirisha misingi inayo hitajika ya maisha ya Kikristo

Waebrania 6:1-2 inasema ***"Mafundisho ya kwanza ya Kristo" (NKJV)* "*Kanuni za mafundisho ya Kristo"* (KJV) Ni***:*

1. "Msingi wa kuzitubia kazi zisizo na uhai,
2. na wa imani kwa Mungu,
3. mafundisho ya mabatizo,
4. kuwekea mikono,
5. wa kufufuliwa wafu,
6. na hukumu ya milele".

Mwandishi wa Waebrania anatuhimiza ***"tuufikilie utimilifu [ukomavu]"*** na anasema ***"na haya tutafanya Mungu akitujalia"* (aya 3).**

Mungu ndiye mjenzi mkuu. Yesu analijenga "***kanisa lake***". ***"Nitalijenga kanisa Langu"* (Mathayo 16:18).** Anasisitiza juu ya misingi imara kuwekwa kabla ya kanisa kukua hadi ukomavu. Mojawapo ya jambo la kuonyesha kukua katika ukomavu ni kuweza kufundisha elimu ya msingi ya Kristo kwa wengine **(Waebrania 5:12).**

Kujua ni kutenda (kusikia na kutii)

Kuzijua kanuni za misingi ya imani inahusisha kuwa na ujuzi wa uhakika wa toba, imani, mabatizo, kuwekea mikono, kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele. Lakini kwanza tunastahili kuwa tumesikia mafundisho ya biblia ya misingi kwa ukweli. Tukisha lisikia neno, kisha tunatii, kisha mtihani wa ukomavu wetu ni kwamba tunaweza kuwafundisha watu wengine misingi hiyo.

Mara kwa mara wale watu wametembea na Bwana kwa muda hawajawahi kusikia maandiko yakifundishwa ya ubatizo wa maji. Wakati wanasikia neno wanashawishika na wanatafuta ubatizo wa maji mengi/wakuzamishwa, hii imeleta utata katika baadhi ya makanisa kwa maana huwa wanafanya ubatizo wa watoto na wanakataa kubatizwa upya.

Ni watu wachache sana kanisani leo wamesikia mahubiri ya mbinguni na kusimu (hukumu ya milelel) lakini Roho Mtakatifu sasa anahimiza fundisho hili. Fundisho lenye mamlaka katika maandiko katika uhakika na asiri ya kuzimu yanatoka kwa Bwana Yesu mwenyewe, katika injili.

Katika makanisa mengine, kuwekewa mikono haifanyiki na inatendeka kwa matukio machache. Ila ni kanuni ya msingi, na hivyo yastahili kufanywa na kanisa. Ni jambo la kawaida la kibiblia kufanya huduma ya kuombeana kwa kuwawekea mikono.

<u>Imani ya biblia</u> ni "kufanya kile Yesu anasema". Tumeitwa katika utiifu.

Luka 6:47-49*: "Kila mtu ajaye kwangu, na kuyasikia maneno yangu na kuyatenda, nitawaonyesha mfano wake. Mfano wake ni mtu ajengaye nyumba, na kuchimba chini sana, na kuweka msingi juu ya mwamba; na kulipokuja gharika, mto uliishukia ile nyumba kwa nguvu, usiweze kuitikisa; kwa kuwa imejengwa vizuri. Lakini yule aliyesikia lakini hakutenda, mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba yake juu ya ardhi pasipokuwa na msingi, mto ukaishukia kwa nguvu, ikaanguka mara; na maangamizo yake nyumba ile yakawa makubwa".*

Kote kote duniani leo watu wanamtafuta Yesu; wanatafuta wokovu; wanatafuta njia ya mbinguni, jinsi ya kujiepusha na kusimu. Ndio, wengi wanajificha na uhakika wa umilele na kujijaza na kuyafuatilia ya dunia, wasiwe na jawabu kamili ya shida zilizo wazunguka, wala wasiwe na uweza wa kukabiliana na hali ngumu katika mioyo yao.

Jawabu ni ipi kwa wale wanaoutafuta ukweli?

Msingi wa kwanza na uliozama sana ni ule wa kuzitubia kazi zisizo na uhai. Neno la Mungu linachimbua ndani ya maisha yetu likituamuru tugeuke tumtazamie Mungu. Tunapogeuka na kuziacha njia zetu Mungu anatupa njia yake ambayo ni Yesu (**Yohana 14:6).** Imani ni kwa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Msingi wa imani huwekwa juu ya toba. Kisha tupo tayari kwa mabatizo: kuzamishwa kwa maji ili kuoshwa dhambi zetu, na kuvunja nguvu zake, na kuzamishwa ndani ya Roho Mtakatifu kupokea nguvu za kushuhudia Yesu na kuyaishi maisha yenye ushindi. Kupitia kuwekea mikono Roho Mtakatifu na Baraka na vipawa anazopatiana vinaachiliwa kwa muumini mpya. Kupitia mabatizo na kuwekea mikono, muumini mpya anapokea nguvu za ufufuo na ana uwezo wa kufahamu fundisho la biblia la kufufuliwa wafu. Hii inaelekeza kwa msingi wa mwisho hukumu ya milele ambayo kimsingi inatupa kuchangamkia hatima ya umilelel wetu, uzima baada ya mauti.

PETRO ANAWEKA MISINGI

Petro alihubiri misingi katika siku ya pentekosti?

Ni mambo yapi manne ambayo Petro alipatia watu walipouliza tufanye nini katika **Mdo 2:38?**

i. _____

ii. _____

iii. _____

iv. _____

Walikuwa wabatizwe kwa sababu gani?

_____

Ubatizo huu ulikuwa mpya. Ulikuwa uwe "***katika jina la Yesu Kristo****" [ona sura ya 4]*
Waumini walikuwa wawe na imani kwa Mungu kwa njia ipi?

_____

_____

Petro alikuwa amewahubiria Kristo (Mdo 2:22-37)

Agizo la nne ili kupokea Roho Mtakatifu ingehusisha kuwekea mikono
Katika kuhubiri kwake, Petero alikuwa ameelezea kufufuka kwa Kristo katika wafu. Soma **Mdo 2:24, 31, 34.** Alikuwa ameweka msingi wa **kufufuliwa wafu.**

Alikuwa amehubiri wazi Kristo akiwa ndiye aliyeketi katika mkono wa kuume wa Mungu (**aya 34).** Yesu Kristo amefufuka katika wafu na Mungu amemfanya muamuzi - amefanywa ***"Bwana na Kristo"*** (**aya 36).**

Ameketi **"*hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako"* (aya 35).**

Mdo 2:28-32: petro ananukuu kutoka kwa nabii Yoeli akionyesha "***siku ile ya Bwana iliyo kuu na iliyo dhahiri"* (aya 20)** iliyo siku ya hukumu kwa mataifa yote. Anawaonya "***jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi"* (aya 40**). Anaongea kuhusu **hukumu ya milele.** Lengo la huduma za biblia ni kanisa lililokomaa, kanisa ambalo lina mtazamo wa Yesu, lenye watu wanaomcha Mungu, watu ambao wanaoisikia sauti ya Roho Mtakatifu bila kusita sita, wakiwa na shina kwenye maandiko; kanisa linalojijenga katika upendo, likiwa na huduma yenye mazao, likiwa limejengwa katika msingi wa utume kama ilivyo funuliwa katika maandiko.

Pamoja hebu tujipatiane katika maombi kulitimiza lengo hili.

KUJENGA JUU YA MWAMBA

Somo la msingi kutoka kwa mafundisho ya Yesu

Tunatambua kwamba wakati jengo linajengwa, umakini mwingi unahitajika katika kuweka msingi, kwa maana kama jenga litatumika, imara na la kudumu, lazima liwe na msingi dhabiti. Watu wote wanaelewa kanuni hii, kwamba msingi unaishikilia nyumba. Kila sehemu ya nyumba inategemea msingi. Mungu alitumia mfano huu kutufundisha ukweli huu wa Kiungu.

Biblia inazungumzia maisha Yetu kama jengo, ***"nyumba yake ni sisi"* (Waebrania 3:6)** na inatuambia msingi ambao maisha yetu yanatakiwa kujengwa juu yake.

Hebu tuchunguze mfano wa nyumba mbili katika **Mathayo 7:24-27** na **Luka 6: 46-49** na tuone ukweli ambao Yesu alikuwa akifundisha kuhusu misingi yetu binafsi.

Anamuitaje mtu ambaye anaichunguza misingi ya nyumba? **(Mathayo 7:24**)

Mtu mwenye hekima anajenga wapi nyumba yake? **(Mathayo 7:24)**

_____

Mwamba unazungumzia nini katika maandiko?

(**Mathayo16:18)**_____

_____

1. Wakati “tumezaliwa mara ya pili”, tunamuita Yesu “Bwana”. Utambulizi huu unamtabulisha yeye kama yule tumemuweka katika uangalizi wa maisha yetu. Yesu anasemaje aje kuhusu kuitikia kwetu kwa kwanza tunapomuita ‘Bwana’?

(Luka 6:46) _____

_____

Tunaweza kusikia na ‘kutotenda’? Tunaweza kumuita Yesu ‘Bwana’ na tusitii?
Tunaweza kulijua Neno na tukose kulitii – kuipuuza misingi ambayo nyumba (maisha yetu) inastahili kujengwa juu yake?

2. Andika hatua tatu za utiifu ambazo Yesu anatupa katika **aya 47:**

_____

Hii ni kusikia ama kulijua neno na kulitii.

3. Katika **aya 48,** Yesu alisema yule mtu asikiaye na kulitenda neno ni kama mtu anayejenga nyumba. Yeye _____ na

_____

“***Kuchimba chini sana”.*** Aliondoa kila kizuizi kati yake na mwamba, alihakikisha ya kwamba amesimama mahali imara. (Hatua hii ya kwanza inahusisha toba, kuchimba sana na kuwa na imani ndani ya Yesu, mwamba wa wokovu wetu.)

4. Ni kwanini nyuma ijengwe kwenye mwamba? (**aya 48):** _____

_____

Wabrania 12:25-29*:* Ni kawaida maisha kuwa na misuko suko, na **aya 25** inatuonya: ***“Angalieni msimkatae yeye anenaye”***

5. Wakati gharika ilipokuja, ni nini kiliitendekea nyumba iliyokuwa imejengwa juu ya mwamba? (**aya 48)** _____

_____

Iliyokuwa imejengwa juu ya ardhi (**aya 49)** _____

_____

Nyumba isio na msingi ilianguka na maangamizi yake yakawa makubwa **(aya 49).**

6. Mwamba huu ni nani? **Zaburi 18:2:** _____

_____

Katika **Isaiya 28:16** Mungu mwenye nguvu asema "***Naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye dhamani, msingi uliyo imara".*** Petro ananukuu kutoka kifungu hiki katika **1Petro 2:6.** Anaendelea kuongea juu ya Yesu akiwa jiwe kuu la pembeni ambaye kanisa linajengwa kwake.

Waefeso 2:19-22: Mtume Paulo ananena kutuhusu kama "***watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho".***

Wakristo wengi hawakui na kukomaa kwa maana misingi hii haijawekwa vyema – sio sawa. Lazima iwekwe kulingana na muundo uliowekwa ***"Aliye vitengeneza vitu vyote ni Mungu"*** **(Waebrania 3:4*)*** na "***Bwana asipoijenga nyumba waijengayo wafanya kazi bure"*** **(Zaburi 127:1).**

Tunao muundo wa ujenzi katika Biblia. Katika mafunzo yafuatayo tutaitazama misingi ambayo inatakiwa kuwekwa vyema ili tukue kibinafsi, na ili kanisa la Yesu Kristo lipate kujengwa katika msingi imara.

Orodhesha misingi sita ambayo imeelezewa katika **Waebrania 6:1-2**

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____
6. _____

KUZITUBIA KAZI ZISIZO NA UHAI

‘Kutubu ni kugeuka kutoka kwa dhambi, kutotii, au uasi na kugeuka umtazamie Bwana’ **(Mathayo 9:13; Luka 5:32).** Kwa njia nyingi ya kawaida, kutubu ni kugeuza mawazo **(Luka 19:8),** ama hisia za majuto kwa sababu ya tabia za zamani **(Mathayo 27:3).** Toba ya kweli ni kuwa na ‘hofu ya Kiungu’ kwa sababu ya dhambi, kitendo cha kugeuka kwa njia uliokuwa ukienda. Toba ya namna hii inaelekeza kwa msingi wa mabadiliko wa mtu katika uhusiano wake na Mungu’. (Hayford, ed., *Hayford’s Bible handbook.* 1995: p.742)

Kazi zisizo na uhai ni gani?

Hizi ni kazi na matendo ya mtu anayeishi bila Mungu na zinaweza kuhusisha dhambi, ama kazi za kidini; kwa hakika hali yoyote ambapo mtu anajiweka katika hali kupingana na Mungu. Kazi zisizo na uhai mara moja zinatutenga na Mungu, na kutenganishwa na Mungu ni kifo. Ni wakati tu tunatambua kutenganishwa kwetu na Mungu tunaona hitaji la kutubu.

Tazama maandiko yafuatayo kwa jawabu na uandike.

Tunastahili kufanya nini kujiepusha na kifo?
Luka 13:3:_____

_____

Dhambi ni nini?
Kwa hakika, inamaanisha “kupoteza shabaha”. Paulo anaeleza aje haya?
Warumi 3:23:_____

_____

Ni nani tuliyemuasi?
Zaburi 51:4

_____

_____

Mungu anaamuru watu kila mahali watubu.
Mdo 17:30_____

_____

_____

Na tunajua ya kwamba ni mapenzi yake watu wote wapate kutubu.
2 Petro 3:9 _____

_____

_____

Yohana mbatizaji alihubiri toba kama maandalizi ya kuja kwa Masihi.
Mathayo 3:2 _____

_____

_____

Yesu anaamuru toba kama njia ya kuingia kwa ufalme wa mbinguni.
Mathayo 4:17_____

_____

_____

Mitume, Petro, na Paulo walihubiri toba ili kuupokea uzima wa milele:
Mariko 6:12: (Mitume)

_____

_____

_____

Mdo 2:38: (**Petro**)

_____

_____

_____

Mdo 20:21: (Paulo)

_____

_____

_____

Kurejesha uhusiano na Mungu, ni lazima tutubu, hivyo ni, kufanya maamuzi ya kujitakia ya kubadilisha mawazo yetu na tumgeukie Mungu na kufanya yale anatuagiza kufanya. Maandiko yanasema, "***wote wametenda dhambi"*** **(Warumi 3:23)**

Soma **1 Yohana 1:8-10** na utambue mstari wa kumi. Hata wakristo wanatakiwa kutubu.

Yakobo 2:10: "*Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote."*

Utimilifu wetu utakuja tukikutana na Yesu, uso kwa uso (**1Yohana 3:2).**

Kazi zisizo na uhai zimenakiliwa kwa maandiko. Soma maandiko na uandike orodha hii.
Mariko 7:21-23: Ni mambo yapi ambayo Yesu anasema hutoka kwa ***"moyo wa mwanadamu" "na kunajisi"***

_____

_____

_____

_____

_____

Warumi 1:29-32*:* Paulo anatukumbusha wakati mtu anachagua kupuuza sheria za Mungu***,*** ***"Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wafanye yasiyowapasa"***

_____

_____

_____

_____

_____

Paulo anaonya kanisa kuhusu nini katika **2 Wakorintho 12:20-21.**

_____

_____

Kutokana na maandiko yafuatayo andika mambo yale ambayo yatatuzuia kuingia katika ufalme wa Mungu.
1Wakorintho 6:9-10

_____

_____

Wagalatia 5:19-21

_____

_____

Yesu anatoa onyo kama hilo katika **Ufunuo 22:14-15**
Kuna orodha ingine katika **Ufunuo 21:8** _____

_____

_____

Yesu anasema sehemu yao itakuwa wapi?_____

_____

Warumi 6:23 inasema nini kuhusu matokeo ya dhambi?_____

_____

Kuhusu **"karama ya Mungu"**

_____

_____

Hebu tumjie Mungu sasa kwa toba kwa maana "kupoteza shabaha", kwa "kupungukiwa na utukufu wa Mungu"- kwa kupungukiwa na kile ambacho Mungu ametukusudia.

Wakolosai 3:5-10: Paulo anatufundisha jinsi ya kuyatenda haya. Katika aya **5, 7, 8** na **9** anatukumbusha kuhusu majukumu yetu **"*Ya kuvua kabisa utu wa kale pamoja na matendo yake"*** kwa sababu **"*kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu*"** (**aya 6),** na **"*mkivaa utu mpya".***

Hebu tuchukue wakati sasa katika maombi ya toba na kukuri dhambi zetu mbele ya Mungu: tukikiri mawazo, hivyo **"*tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila filkira ipate kumtii Kristo"* (2 Wakorintho 10:5).**

TOBA IKIELEKEZA KWA IMANI

Hofu ya kiungu huelekeza kwa toba.

Ni wakati tunapotambua ya kuwa dhambi zetu zimemuudhi Mungu na kututenga naye ambapo tunasikia hofu hii ya kiungu. (Ukilinganisha, hofu ya dunia ni ili ambayo tunaihisi tunapotambua kwamba tumejiletea hukumu juu yetu kwa sababu ya dhambi zetu. Tunayalipia makosa yetu na wengine wanateseka pia).

Hofu ya kiungu huelekeza wapi?

2 Wakorintho 7:10 _____

_____

Hofu ya kiungu huelekeza kukiri

Tunachagua kukiri. Tunaamua kugeuka kutoka kwa dhambi kwa mawazo yetu, kisha tunafungua vinywa vyetu na kukiri – kwa mfano tunakubali dhambi zetu. Ni ahadi gani ambayo Mungu huwapatia wale wamekiri dhambi zao?

1 Yohana 1:9: _____

_____

Kutubu na kukiri zinaenda pamoja mara kwa mara katika maandiko

Zote zinahusisha kugeuka kuachana na kitu na kugeuka kuitazama njia mpya. **Mdo 3:19:** ***"Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana."*** Haijatosha tu kukiri dhambi zetu tu. Toba inahusisha kugeuza kwa mawazo ambapo tunageuka kikamilifu kutoka kwa yale tumekuwa tukiyatenda na kugeuka kuyatenda yale Mungu angelipenda tuyatende.

Hii imeelezwa katika **Luka 22:32.** Wakati yesu aliongea na petro: _____

_____

_____

Hadithi ya mwana mpotevu katika **Luka 15:11-24** inaonyesha kukiri na kugeuka.

Yule mwana – ***"alizingatia moyoni mwake"*** **(aya 17) -** kuitikia kwa sababu ya hofu ya dunia.

- Alifanya maamuzi (**aya 18-19**) **-** alitubu kutoka kwa mawazo
- Alifanya kulingana na maazimio yake **(aya 20) -** aligeuka.

Maamuzi ya mapenzi yake yalielekeza kuchukua hatua na hofu yake ya dunia ikageuka kuwa hofu ya Mungu. Kama vile baba katika hadithi katika **Luka 15** alimpokea mwanawe kwa upendo na furaha, hivyo Mungu humpokea mwenye dhambi aliyetubu.

Matokeo ya toba ya kweli ni gani?

(a) Upendo mpya kwa Mungu na jitihada za kuyaishi maisha ya haki ambayo ametupatia

Ni kwa nini tunaweza kupata haki hii?

1Petro 2:24 _____

_____

_____

2 Wakorintho 5:21 _____

_____

_____

Huwa tunabaki kwa hali ya kuwa haki kwa jinsi gani?

Warumi 12:1-2 _____

_____

Warumi 6:13 _____

_____

Kifungu hiki chaonyesha mfano "kugeuka kutoka kwa" na "kule kugeukia" (kutazama) ambayo toba inaelezea.

(b) Uhuru kutoka kwa dhambi

Tunakiri dhambi na kupokea ahadi na msamaha kutoka kwa Mungu **(1 Yohana 1:9)**

Tokeo moja ni lipi ya kupokea msamaha huu na haki kutoka kwa Mungu?
Warumi 8:1 _____

_____

(c) Upendo kwa haki na maadili.

Paulo anaeleza haya kwa njia gani katika **Waefeso 4:22-24** _____

_____

_____

_____

na katika **Wakolosai 1:22**_____

_____

_____

(d) Amani mpya na furaha katika kuishi maisha ambayo ni ya kumtazama Mungu

Andika Baraka za Yesu katika **Yohana 14:27** _____

_____

_____

za Paulo katika **Warumi 15:13** _____

_____

na baraka ambazo zinatokana na kutii kama Paulo anavyohimiza katika Wafilipi 4:6-7:

_____

_____

Elewa kwamba matokeo ya toba yanakuja wakati tunaishi maisha ya kumtazamia Yesu. Toba inahusishwa na mambo mengine ya maisha ya Ukristo, ambayo yanaelekeza katika ukomavu.

- Ni nini Yesu alishikanisha na Toba? **Mariko 1:15** _____
- Ni nini Ptero alishikanisha na Toba? **Mdo 2:38** _____

  Mdo 3:19 _____
- Ni nini Paulo alisema inadhibitisha kutubu kwao? **Mdo 26:20** _____

  _____
- Ni nini Yesu aliamuru viongozi wa dini wa siku yake kufanya kilicho lingana na toba?

  Mathayo 3:8 _____

  _____

Kutubu ni karama kutoka kwa Mungu.
2 Timotheo 2:25 _____

_____

Yesu alikuja kutuita katika toba
Mathayo 9:13 _____

_____

Karama nikwa watu wote.
Mdo 11:18 _____

_____

Yesu ametutuma kuhubiri toba na msamaha wa dhambi katika jina lake kwa mataifa yote.
Luka 24:47 _____

_____

Ni kwa imani ndani ya Mungu ambapo tunapokea toba

KUJIFUNDISHA NENO

Neno kuu katika **kutubu** katika Kiyunani katika Agano Jipya ni **metanoia,** kimsingi ikimaanisha: kinachokuja baada ya mafikira, kuyabadirisha mawazo. *Meta* yamaanisha baada, ikileta mabadiliko, na *nous* ni mawazo, kiti cha mtazamo wa tabia (Vines, 961- 962). *(Vines* 963) inaendelea kusema katika Agano Jipya, neno hili, *"haswa lina mtazamo wa kutubu kutoka kwa dhambi, na mabadiliko haya ya mawazo inahusisha kumgeukia Mungu"*

Ifuatayo ni orodha ya maneno na maana yake ambayo yanatumika katika biblia kuelezea ambacho kinahitajika ili tutubu kutoka. Maneno ya Kiyunani yametolewa kutoka kwa *vine's Expository Dictionary ya Agano la kale na jipya,* World Bible Publisher, lowa Falls, lowa.

Dhambi: *harmatia:* kupoteza shabaha
hamartia: kitendo cha kutotii sheria za Kiungu

Uovu: *kakos:* inasimamia kila kilicho kiovu katika tabia. Inaonyesha kilicho bure kisicho na uweza, kibaya
Poneros: inamaanisha kinacho leta uharibifu, majeraha, uovu, inayotumika kwa usemi, mawazo ya mwanadamu.

Uasi: *Poneria:* uasi
kakia: uasi, chafu, kitu cha kudhuru

Makosa: *parabasis:* kimsingi kwenda kando, kwenda Zaidi, (inamaanisha kuvunja sheria)

Udhalimu: *adikia*: mambo yasio ya haki, uovu, matendo yanayo hukumu sheria na haki.

Kutomcha Mungu: *asebia:* kutomheshimu Mungu, kuto kuwa na Uungu, ni kile kitendo cha kutotambua au uasi wa utu wa Mungu

Uovu: *anomia:* uasi -sheria

Kutotii: *apeitheia:* inamaanisha kukataa mapenzi ya Mungu.
parakoe: kimsingi kukosea katika kusikia, ikionyesa ile hali ya kukataa kusikia, ikileta kitendo cha kutotii.

Kosa: *paraptoma:* hatua ya uongo, ikionyesha kupotoka kutoka kwa unyoofu na ukweli.

IMANI KWA MUNGU

Imani (pistis) ni hali ya kuwa na ushawishi mkuu, kushawishika kunakotokana na kusikia, katika Agano Jipya kila mara inatumika kuonyesha imani kwa Mungu ama Kristo ama vitu vya kiroho. Inahusisha kuamini na kutumaini. Imani ni kumtegemea Kristo Yesu kwa wokovu. Imani inarejelea ukweli ambao tunaamini (Yuda 3).

Kuwa na imani ni lazima tuamini na tutumaini. Pakiwa na imani, kuna mengi yanahusika ila tu kuwa na maoni. Ni kwa sababu Paulo anatumaini Mungu na ana imani na yale Yesu ametenda anaweza kusema, ***"Nimekwisha kujua vyema hakika…"*** **Warumi 8:38**

Kama tulivyoona na kutambua dhambi – kupoteza shabaha na kupungukiwa na utukufu wa Mungu - tukapata hofu ya Mungu na tukaokoka. Lakini tusipoamini kwamba tumesamehewa, toba hii ni ya bure. **Kutubu na imani zinaenda moja kwa moja.** Tusipo mtumaini Mungu kuondoa dhambi zetu, hukumu na aibu, na kuamini kwamba Yesu ametenda haya kwetu, juhudi zetu za kuacha (kuwa huru) na dhambi zitaambulia patupu. Na vile vile tutakuwa wanafiki tukisema tumemgeukia Mungu na kuendelea na dhambi (Au kubaki katika dhambi zetu). **Kutubu inahusisha kugeuka kutoka kwa dhambi na kumgeukia Mungu kwa imani.**

Ufafanuzi wa imani:
"Ni kile kitendo ambacho mtu anakumbatia rasilimali ya Mungu, na kutii yale Mungu anaelezea, na kuacha mambo yote ya ubinafsi, na hali ya kujitegemea kumtumaini Mungu kikamilifu." (W.A. White house)

Biblia inaeleza imani kwa njia gani?

Waebrania 11:1 _____

_____

_____

Tunaamini kwamba yale mambo ambayo Mungu ameahidi yatakuja kutokea. Tunaamini Mungu ***"anaweza kuyafanya yale aliyoahidi"*** na ***"huku akijua hakika, ya kuwa Mungu aweza kuyetenda"*** **(Warumi 4:21).** Haya sio mawazo mema au kutamani mema. Hii ni kuamini na kutumaini kwamba Mungu anaweza kutenda alicho ahidi. Hii ni imani katika Mungu. Yanayokuja na yale yasiooneka na yanayokuja hakika kwa sababu tunamtumaini Mungu.
"*imani kupokea kwa hakika ambacho hakijafichuliwa kwa fikira"* (Waebrania 11:1 Amplified Bible).

Mtu hawezi kuokoka pasipo imani. (Andika maandiko yafuatayo)
Mariko 16:16 _____

_____

_____

Luka 8:12 _____

_____

_____

1Wakorintho 1:21 _____

_____

_____

Waefeso 2:8 _____

_____

_____

Mtu hawezi kumpendeza Mungu pasipokuwa na imani.
Waebrania 11:6_____

_____

_____

TWAPOKEA AJE IMANI?
Warumi 10:17 _____

_____

_____

Ukristo ni imani iliyofunuliwa. Mungu anaendelea kutaka kunena nasi.
Paulo anamwambia aje Timotheo kuhusu maandiko
2 Timotheo 3:16 _____

_____

Neno la Mungu ni vile linasema. Ni Mungu akisema nasi.
Yesu alisema***, "Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu"*** **(Mathayo 4:4).**

Ni wakati tunasikia maneno ambayo Mungu ananena kwetu binafsi ambapo tunapokea imani ya kutenda na kuishi nayo. Hili ni neno "lililohuishwa/Rhema" ambayo Mungu analeta uhai katika hali fulani. Watu wengi wamekuja katika imani ndani ya Yesu Kristo wanaposoma Biblia na wakasikia Mungu akiwanenea. Yesu anakuwa dhahili kwao. Yeye "***ndiye neno lililo fanyika mwili"*** **(Yohana 1:14).**

Katika Agano jipya ya Kiyunani, yapo maneno mawili muhimu ambayo yanatafsiriwa kwa kingereza kama "neno": **Logos na Rhema. Logos** ni biblia, neno lililoandikwa la Mungu***;*** ***Rhema*** ni neno "lililohuishwa" la Mungu.

Kama tusomavyo Biblia tunabadilishwa tunapomsikia Mungu akisema nasi.
Ni nini kilicho tendeka wakati watu walisikia Petro na Yohana wakinena?
Mdo 4:4_____

_____

Watu wa Samalia walipo muamini Filipo, walitii.
Mdo 8:12: _____

_____

_____

Katika kujaribiwa kwake Paulo alionyesha imani yake katika neno la Mungu kama ilivyo funuliwa katika sheria na manabii. **Alikuwa akielezea kwamba ameamini kwamba Mungu alikuwa akimzungumzia kupitia maandiko.**
Mdo 24:14 __________

_____

Kuwa na habari tu haihakikishi wokovu.
Yakobo 2:19_____

_____

Wangi wana mawazo yenye habari na hisia zilizo sisimuka wakati wanapo lisikia neno la Mungu. Hata tunapolisikia neno na mioyo yetu inaitikia kwa furaha kwa wakati huo, tungali tunatakiwa kuchagua kupokea na kuitikia Yule ambaye amenena kwa mioyo yetu. **Tunamgeukia Mungu na kubadilika tunapomtumaini kwa kulitimiza neno lake kwetu na kutambua kwamba Mungu ni muaminifu na huweka ahadi zake (Zaburi 145:13).**
Huku kumgeukia Mungu katika imani kunatuadhiri kwa njia gani?
Wafilipi 1:25 _____

_____

Watu walipokea neno la Petro kwa njia gani katika **Mdo 2:41 _____**

_____ na Filipo **Mdo 8:8?** _____

_____

Je, ujumbe katika **1 Wathesalonike 1:6** ulipokelewa? _____

_____

1 Petro 1:8 pia inazungumza juu ya "***nakufurahia sana, kwa furaha isiyoneneka".***

IBRAHIMU – BABA WA WOTE WANAOAMINI

Katika **Warumi 4** Paulo anaandika kuhusu Ibrahimu kuelezea imani. Ni kwa nini Mungu alimhesabia Ibrahimu kuwa haki? **(Aya 3**) _____

(a) Aya 13,21 inaongea kuhusu Ibrahimu **akipokea neno – kusikia neno.**

(b) Aya 18-20 inaonyesa akikataa au **kugeuka kwa imani kutoka kwa hali yake isiyokuwa na tumaini.**

(c) Aya18 inaonyesha Ibrahimu akikumbatia tumaini ikielezewa kwa ahadi ya kiungu ambayo alipewa katika **Mwanzo 15:3-6.**

(d) Hakusita katika kujipatiana kwake aya 20.

(e) "Alimtukuza Mungu" na akafurahia kwa yale ambayo yalikuwa mbele yake – aya 20

Paulo anawaitaje wale wanaoamini? **Wagalatia 3:7** _____

_____

na hua tunapokea nini? **Wagalatia 3:9**_____

_____

Soma **Waebrania 11** na kwa mstari mmoja ama miwili, sema ni kwa nini kila mmoja wa hawa ***"alipongezwa"*** kwa sababu ya imani yao **aya 39**

[kwa mfano waliamini Mungu, na maono ama neno aliowapa, wakiteseka na wakati mwingine wakifa katika imani bila kuona ahadi zikitimizwa katika siku zao.]

_____

_____

_____

_____

_____

_____

IMANI KWA MUNGU KUPITIA YESU KRISTO

Wabrania 11:39-40 ***"Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi".***

Yesu ni utimilifu wa "***kitu kilicho bora"*** ambacho Mungu alikuwa ametupangia. Kila ahadi katika Agano la kale limetimizwa katika Kristo Yesu.

Ufafanuzi wa Charles Finney wa imani: "Ni ile hali ya kumpokea Kristo kwa kile ambacho ameakilishwa kuwa katika injili yake, na kujipatiana kusiko hitimu kwa mapenzi, na kwa utu wote wake".

Katika maisha yake ya duniani Yesu alimtazama Baba. Maisha yake ya dunia ilikuwa ni ushuhuda kwa Mungu. Wakati Yesu alifanya mujiza wake wa kwanza kwa harusi katika Kana, ***"mwanzo huo wa ishara Yesu alifanya katika Kana ya Galilaya, ukaudhirisha utukufu wake, nao wanafunzi wake wakamuamini."*** **(Yohana 2:11)**

Yesu aliwajibu namna gani walipomuuliza, ***"Basi tufanye aje tupate kuzitenda kazi za Mungu"?*** **Yohana 6:29** _____

_____

Yesu alisema nini kwa Tomaso? **Yohana 14:7** _____

_____

Yesu alisema nini kwa Filipo wakati aliposema, **"*Tuonyeshe Baba"?* Yohana 14:9-14**

Aya. 10 _____

Aya.11_____

Aya .12 _____

_____

Aya .13 _____

Aya. 14 _____

Yesu alisema nini alipotenda miujiza ya uponyaji? **Mathayo 8:13** _____

_____

Mathayo 9:22_____

_____

Mathayo 9:29_____

_____

Wakati wanafunzi waliona muujiza wa mkuyu uliokauka?

Mariko 11:22-23_____

_____

Maisha yake ya kufufuka ulikuwa ni ushuhuda wa nguvu za Mungu.

Hizi nguvu zilizo mfufua Yesu kutoka kwa wafu zinapatikana kwa wale waaminio. (**Waefeso 1:19-23).**

Andika kile ambacho Paulo anasema: **1 Wakorintho 2:5** _____

_____

1 Wakorintho 15:17: ***"Na kama Kristo hakufufuka, imani Yetu ni bure; mngalipo katika dhambi zenu".***

Soma **Yohana 20:29-31.** Yesu alisema nini kwa Tomaso kuhusu kuamini? **aya 29**

_____

Ni yapi matokeo ya kuamini? **(Aya .31)**

Ni kwa **"*imani tunasimama"* (2 Wakorintho 1:24).**
Yesu anataka tuamini "ndani ya mioyo yetu" na tusiwe na shaka. **Yakobo 1:6** inatupa onyo kama ile.

Ni nini tunapokea kwa imani kutoka kwa Yesu.

(a) Ahadi ya Roho Mtakatifu – Wagalatia 3:14

(b) Hali ya Kufanyika wana – Wagalatia 3:26

(c) <u>Wokovu – Waefeso 2:8</u>

(d) <u>Kumfikia Baba – Waefeso 3:12</u>

Paulo anasema **"*tukishahesabiwa haki itokayo katika imani"*** sasa **"*na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. Ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo tunasimama ndani yake"* (Warumi 5:1-2)**

Muandishi wa Waebrania anatuambia tusongee kwa ujasiri katika uwepo wa Mungu kwa sababu Yesu ametufanyia njia kupitia dhabihu yake msarabani.
Waebrania 10:19-23: Anasemaje tunaweza kumkaribia?
(Aya 22)
Ni kwa nini tunaweza kufanya hayo?
(Aya. 23)

(e) <u>Ushindi</u>
Sisi ni washindi kwa njia gani?
Ufunuo 12:11

1Yohana 5:4

Ibrahimu **"*alijua kwa hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi*" (Warumi 4:21)** na **"*kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa haki*" (aya 22).** Maandiko yanasema ya kwamba **"*wenye haki wataishi kwa imani*" (Warumi 1:17).**

Tumeuweka msingi wa kutubu ndani ya **maisha** yetu na kwa hivyo **"*nimepati haki na Mungu*"** kupitia Yesu Kristo **(Wafilipi3:9).** Mungu anataka nasi pia, tuishi kama Ibrahimu, ***"tukishawishika kabisa kwamba kile alichoahidi pia ana uweza wa kufanya"***

Hebu sasa pamoja na Petro tufurahie na tuseme **"*Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kweke Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu uliyo tayari kufunuliwa wakati wa mwisho. Mnafurahi sana wakati huu, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo. Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu*" 1Petro 1:3-8.**

MAFUNDISHO YA MABATIZO

Maandiko yananena kuhusu mabatizo nne:

1. Ubatizo wa maji,
2. Kubatizwa kwa ama ndani ya Roho Mtakatifu
3. Ubatizo wa moto
4. Ubatizo ndani ya mwili wa Kristo (**1Wakorintho 12:13**), [pengine ikimaanisha ubatizo wa Roho]; na ubatizo wa tano ni ule ambao haujatajwa: **Luka 12:50** na **Mariko 10:38,** unaojulikana kama ubatizo wa mateso.

Fundisho la mabatizo katiaka **Waebrania 6:2** haswa inazungumzia ubatizo wa maji. Neno la Kiyunani liko katika wingi na linatafsiriwa pahali pengine kama "kuoshwa". Pahali pengine na hapa; inazungumzia sherehe za kuoswa chini ya torati ya Musa na tabia za wayahudi. Pia inahusisha ubatizo wa Yohana na tabia za Kiyahudi za kuwabatiza ambao walikuwa wanajiunga na dini ya kiyahudi, hivyo ni waliogeuka kujiunga na dini ya kiyahudi kutoka kwa wapagani.

Tabia ya ubatizo haikuwa mpya kabisa wakati Yohana alikuja lakini lililokuwa jipya ni wahahudi kubatizwa ikiwa ni ishara ya toba. Walikuwa wakidhani ni mataifa peke yao walihitaji kutubu na kumwamini Mungu wa kweli.

Kubatizwa haswa inamaanisha kuzamishwa: kubatiza ni kuzamisha ama kusafisha na msingi wa neno hili ni kutupukiza, kufunikwa, mfano kufunikwa kwa maji.

1. UBATIZO WA YESU

Yesu alibatizwa na Yohana, sio ishara ya kutubu lakini kutimiza **"*haki yote"***
Mathayo 3:15_____

_____

_____

Ubatizo wa Yesu (sherehe ya kuoshwa ya makuhani katika miaka thelathini) ilikuwa ikifuatwa na upako, kwa njia ya Kiungu na Roho Mtakatifu.
Mathayo 3:16_____

_____

_____

Mara Yesu alipobatizwa, huduma ya Yohana ilianza kupungua na huduma ya Yesu kuongezeka kwa njia kuu. Yohana alikuwa amemtanguliza Masihi kwa Israeli.

Yohana 4:1-2_____

_____

_____

_____

2. AMRI YA KUBATIZA

Amri hii inatoka kwa Yesu mwenyewe, Yesu aliwaagiza wanafunzi "***Basi, enendeni, mkawafanye wanafunzi … mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu"*** **(Mt 28:19),** hivyo ni, katika utimilifu wote wa Bwana Yesu Kristo**.**
Yesu anaiweka wazi kabisa kwamba ubatizo huu hufuata kuamini.

Ubatizo unatanguliwa na:

a) **Kutubu** (Kubadilika): **Luka 24:47** _____

_____

b) **Imani: Mk.16:16** _____

_____

Toba ya kweli (kubadilika) inatangulia imani ya kuokoka. Mtu ambaye amebatizwa anatakiwa awe mtu (aliyebadilika) na mtu wa kuamini kwanza. (Konner, 1973:p.39)

Mtoto mchanga hawezi kutubu wala kuamini. Kwa hivyo ubatizo wa watoto hautambuliki kwa sababu haitimizi haki.

3. TABIA ZA UBATIZO KATIKA KITABU CHA MATENDO YA MITUME

- **Siku ya pentekosti -** Soma **Mdo 2:37-41**

Wakati wa kuzaliwa kwa kanisa siku ya pentekosti, Roho Mtakatifu aliwashawishi wale ambao waliona kile kilifanyika na wakasikia kile Petro alihubiri na wakasema:
Aya .37: *"Tutendeje?*
Petro alijibu kulingana na maagizo ya Yesu: **Aya. 38*: tubuni mkabatizwe***

Ni nini kilitendeka
Aya 41. Nao waliolipokea neno lake walibatizwa– na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. [Kumbuka: waliamuriwa kubaizwa katika Jina la Yesu Kristo.]

- **Katika Samaria -** Soma **Mdo 8:5-8** na **8:14-17**

Aya. 12*:* waliomwamini Filipo, akihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na Jina lake Yesu Kristio, wakabatizwa waume na wanawake
Aya. 16: Wamebatizwa kwa Jina la Bwana Yesu. Walikuwa hawajashukiwa na Roho Mtakatifu.

- **Yule mtu wa kushi -** Soma **Mdo 8:35-38**

Ni vipengele vipi muhimu katika ubatizo?

i. Anasoma neno la Mungu;
ii. Alikuwa anataka na kutamani kuelewa maandiko;
iii. Anamuamini Yesu mara anasikia;
iv. Anabatizwa mara kwa msingi wa imani katika Yesu Kristo kama Mwana wa Mungu.

- **Sauli katika Dameski -** Soma **Mdo 9:17-18**

Sauli anapokea ufunuo wa Yesu Kristo na anabatizwa na Anania.

- **Watu wa mataifa wanabatizwa** - Soma **Mdo 10:44-48**

Ni vipengele zipi muhimu hapa?

i. _____
ii. _____
iii. _____
iv. _____

Je mpangilio wa kawaida wa maandiko unafuatwa?

- **Paul katika Efeso -** Soma **Mdo 19:1-7**

Kuna aina mbili za ubatizo hapa.
Ni zipi?

- **Aya 4**. ubatizo wa toba (ubatizo wa Yohana)
- **Aya 5**. Kubatizwa tena yenye msingi kwenye imani katika Yesu Kristo ambaye huondoa dhambi.
- **Aya 6**. Baada ya haya Roho Mtakatifu anawashukia kupitia kuwekewa mikono na Paulo.

- **Waumini wapya walibatizwa lini katika Agano Jipya?**

i. **Mdo 2:41**_____
ii. **Mdo 8:12**_____
Mdo 8:37-38_____
iii. **Mdo 16:33**_____

4. UBATIZO WA WAKRISTO.

Fundisho la mabatizo katika nyaraka.

Kuonyesha picha ya ubatizo wa wakristo: agizo la kubatiza waamini wapya ilipeanwa na Yesu baada ya kufa, kuzikwa na kufufuka. Mitume na wanafubzi walitekeleza ubatizo wa maji baada ya kufufuka kwake na kutukuzwa. Alikuwa amefanyika kuwa **"*Bwana na Kristo"*** (**Mdo 2:36**). Sasa yeye ndiye Bwana Yesu Kristo.

Ubatizo wa wakristo kimsingi sio wa toba lakini inahusisha toba na ni kwa msingi wa imani katika Yesu Kristo.

Ubatizo wa wakristo sio kuzaliwa upya, huwa inakuja baada ya kuzaliwa upya kwa imani katika Yesu Kristo.

Wakati mtu amezaliwa mara ya pili wamekuwa viumbe vipya; ya kale yamepita **(2 Wakorintho 5:17).** Mfuasi wa Yesu hubeba msaraba wake na kumfuata Yesu. Hatua ya kwanza ni imani (Utiifu) ikifuatwa na ubatizo wa maji (**Mariko 16:16).**

Kutabulishwa na Yesu Kristo katika ubatizo

Warumi 6:3*:* kifo _____

_____

Warumi 6:4*:* kuzikwa:_____

_____

Kufufuka:_____

_____

Warumi 6:5: Tutaunganika katika mfano wa mauti yake
Kuunganika katika mfano wa kufufuka kwake
Warumi 6:6: Utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye
Warumi 6:7*:* Tumehesabiwa haki mbali na dhambi
Warumi 6:8: Tulikufa pamoja na Yesu
Tunaishi pamoja naye
Warumi 6:9*:* Ameshinda mauti
Warumi 6:10: Aliifia dhambi mara moja tu, lakini kwa kule kuishi kwake, amuishia Mungu

Kuzamishwa ndani ya Kristo

1 Wakorintho 10:1-4*:* Baba zetu walibatizwa ndani ya Musa katika wingu na bahari; hata hivyo, **Wagalatia 3:27,** tulibatizwa katika Kristo na tumejivika ama kuvaa Kristo, tunapatikana ndani yake.

Ubatizo wa wakristo haungekuwa tofauti na ubatizo wa Yohana kama Yesu hangekufa na kufufuka tena. **1Petro 3:21**: Wakati tumebatizwa katika Kristo tunabatizwa katika Kristo aliye fufuka. Imani ndani yake kupitia ubatizo ndio jawabu ya dhamiri nzuri kwa Mungu.

Ni damu ya Kristo ambayo inafanya ubatizo wa wakristo kuwa dhahiri

1Yohana 5:6*:* Yesu alikuja kwa maji na damu, sio tu kwa maji bali kwa maji na damu. Sherehe zote za kuoshwa ikihusisha ya Yohana ya toba hazingeosha dhambi ya mtu. Kila aina ya kuoshwa iliyotangulia (mabatizo) zilikuwa sherehe, ishara, zikielekeza, na ikingonjea ile halisi itokee. Yesu alikuja kwa maji na damu; pasipo mwagiko la damu hapana msamaha wa dhambi (**Waebrania 9:22).** Ubatizo wa wakristo unaonyesha **"kuoshwa kwa dhambi"** kwa maana yule mtu anabatizwa ameshapokea msamaha kupitia damu yake.

Mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu

Tambua kwamba Yesu aliamuru kwamba wabatize **"kwa jina":** ni jina lipi ambalo linamfunua Baba, Mwana na Roho Mtakatifu? Ni maneno yapi yanatakiwa kunenwa wakati wa ubatizo?

Mdo. 2:38_____

Mdo. 8:12_____

Mdo. 19:5_____

Petro alisema wabatize kwa jina la Yesu Kristo

Petro ndiye mtume aliyekuwa na wale kumi na mmoja wakati Yesu aliwapa maagizo ya **Mt 28:19**. Hapa ndani kuna siri! Mengi ya makanisa leo na kote katika historia wametumia maneno ya **Mathayo 28:19** katika ubatizo, ila hali **Petro alisema wazi wabatize kwa jina la Bwana Yesu. Petro alikuwa na kutotii?** Ama **Petro alipokea ufunuo wa jina lililofunuliwa la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu?** Kwa wazi wote wanakubaliana kwamab jina la Mwana ni Yesu, **(Mathayo 1:21)**

Jina la Baba ni gani?

Baba peke yake sio jina ka kibinafsi, lakini linaeleza wajibu ama utekelezaji wa mtu katika mahusiano. Katika **Kutoka 3:14** Mungu alidhihirisha jina lake kwa Musa kama"***Mimi niko"*** na jina hili limetafsiriwa kwa wingi katika Biblia ya Kingereza kama "**BWANA",** lakini mara ingine kama **Yehovah** ama **Yahweh.**

Roho Mtakatifu anaelezwa kwa jia nyingi

Hakuna mahali katika biblia ambapo kuna jina lililofunuliwa la Roho mtakatifu. Kristo inamaanisha '**aliyepakwa'** ikionyesha kule kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu aliyemjia Yesu kumwezesha kufanya kazi katika huduma na kutimiza wajibu wake kama Masihi **(Mdo10:38)**. Kwa hivyo kwa hakika jina lililofunuliwa la Baba ni BWANA, na Mungu amemfanya huyu Yesu, Mwana, kuwa Bwana na Masihi **(Mdo 2:36).** Utabulizi **'Kristo',** ambao ni sawa na **'Masihi'** unazungumzia **Roho Mtakatifu ambaye alimjia Yesu , akimpaka awe Masihi.**

Jina la Yesu liko juu ya majina yote!

Maana katika yeye, utimilifu wote wa Mungu unakaa kwa jinsi ya Mwili (Wakolosai 2:9). Hii inamaanisha ya kuwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu wanadhihirika katika Masihi. **Wafilipi 2:11** "***na kila ulimi ukiri ya kuwa, YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba".* Jina la Yesu ndilo alilopewa na Mungu lililo juu ya majina yote, Aya 9.** Ndiposa Petro alibatiza kwa jina la Yesu Kristo. Mtume Paulo alikuwa na ufunuo huo pia alipowabatiza waumini katika **Mdo 19:5** "***Katika Jina la Bwana Yesu".***

Mdo 4:10 na12*: "Hakuna jina lingine"!*

Mzee mwenye hekima wakati mmoja alielekeza muumini mchanga: kujiepusha na ubishi mizozo, fuata mfano huu katika kujipatiana kwa ubatizo wa watu "Katika kukiri kwako kwa imani: kwa utukufu wa Mungu, Mwana na Roho Mtakatifu, tunakubatiza kwa jina la Bwana Yesu Kristo.

KILA ATAKAYEAMINI NA KUBATIZWA UTAOKOKA (Mariko 16:16)

KUWEKEA MIKONO

Mara tu muumini ametubu na kumgeukia Mungu kupitia imani kwa Yesu Kristo; na amebatizwa katika kutii maagizo ya Yesu, hatua inayofuata ya ukomavu ni **kujazwa na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu,** "ahadi ya baba" **(Luka 2:49)**

Ila na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa jia ya kiungu juu ya waumini wa Kiyahudi katika siku ya Pentekosti **(Mdo 2:4)** na juu ya watu wa mataifa waliokutana kwa nyumba ya Kornelio wakati Petro alihubiri katika **(Mdo 10:44) karama ya Roho Mtakatifu ilikuwa imeachiliwa kwa waumini kupitia kuwekea mikono.**

Mara muumini amepokea Roho Mtakatifu katika jia ya kujazwa na kutiwa nguvu, karama zote za Roho zinaweza kupatikana kwa muumini, kwa maana Roho Mtakatifu amekuja na kukaa na muumini. Hata hivyo baadhi ya karama zingine kwa waumini zinaachiliwa kwa kuwekea mikono.

Katika sehemu hii tutajifundisha kuona jinsi Mungu amepatiana karama zake za Roho Mtakatifu kanisani na kuendelea kufanya hivyo kwa njia ya kuwekea mikono ili kuliwezesha kanisa kukua (kuufikia utimilifu) na kulitimiza kusudi la Mungu.

Katika Agano la Kale kuwekea mikono ilikuwa ikihusika na:

A. Baraka ya kutoa ya kiunabii
B. Kuwekwa wakfu kwa sababu ya huduma

Katika Agano Jipya kuwekea mikono inahusika na:

A. Huduma ya Yesu – matokeo yakiwa uponyaji na Baraka
B. Maisha ya kanisa la kwanza wakati waunmini wa Yesu

- Wanabatizwa na Roho Mtakatifu
- Wanawekwa wakfu katika huduma
- Wanahudumu uponyaji kwa njia ya nguvu za Roho Mtakatifu.

MIFANO YA AGANO LA KALE YA KUWEKEA MIKONO.

A. Baraka ya kutoa ya kiunabii.

Katika Agano la Kale, kwa kuwekewa mikono, watu wa Mungu waliitwa kuwa baraka ambayo, ilitambua ile ahadi ya agano ya Mungu kwa baba zao na ilifuatwa na neno la kiunabii la ahadi za baadaye. Pia kwa hiki kitendo urithi ulikuwa ukiwekwa muhuri kisheria.

Yakobo anawabariki wana wa Yusufu kwa kuwawekea mikono. Yusufu alitarajia baba yake aweke mikono yake kwa vichwa vya hao vijana kwa sababu aliwaweka pahali panapostahili ili Yakobo afanye hivyo na kwa mzaliwa wa kwanza apokee baraka ya urithi.

Mwanzo 48:14-16*:* Yakobo alimuitia Mungu abariki wakati aliwawekea vijana mikono na akanena kiunabii yatakayojili kwa mataifa.

B. Kuweka wakfu kwa ajili ya huduma.

Soma **Hesabu 27:15-23.**

Ni nini Mungu aliagiza Musa kufanya katika majibu ya ombi lake katika **aya 16-17?**

Aya. 18:_____

Aya. 20:_____

Musa aliyafanyia haya wapi?

Aya 22:_____

Hapa tunaona:

a) Kuwekea mikono
b) Kutoa kwa mamlaka
c) Kuwekwa wakfu mbele ya mashahidi

Kumbukumbu 34:9 inasema nini kuhusu tukio hili? _____

_____

Katika kutumwa huku kwa hadhala kwa Yoshua, Musa alimuwekea mikono na akatoa ama kuhamisha baadhi ya mamlaka juu yake **(Hesabu 27:20),** kama ishara kwa taifa ambalo Mungu alitambua mamlaka ya Yoshua.

Hesabu 8:10-11*:* Mungu pia alimuagiza Musa kuwaleta Walawi mbele yake na ***"Kisha wana wa Israeli wataweka mikono yao juu ya Walawi…ili wawe wenye kufanya utumishi wa BWANA".***

MFANO WA AGANO JIPYA WA KUWEKEA MIKONO.

A. <u>Katika maisha ya Yesu</u>

1. Huduma yake ya uponyaji.

Matarajio ya mtawala yalikuwa yapi alipokuja kwa Yesu? **Mathayo 9:18**

_____

_____

Ni nini kilitendeka wakati Yesu aliwawekea watu wachache wagonjwa mikono? **Mariko 6:5**

_____

_____

Kwa kila mtu? **Luka 4:40** _____

_____

Kwa yule mwanamke kiwete? **Luka 13:13** _____

_____

2. Yesu aliwabariki watoto.

Ni kwa nini watoto waliletwa kwa Yesu? **Mathayo 19:13**

_____

_____

Majibu yalikuwa yapi? **Aya 15:** _____

_____

3. Yesu aliagiza waumini kuwawekea wagonjwa mikono.

Amri yake kwa kanisa ni gani? **Mariko 16:18**

_____

_____

Alijibu kwa jinsi gani kwa wale waliomtii na kumtumaini? **Aya 20**

_____

_____

Ni ahadi ipi ambayo Yesu ametuahidi katika **Yohane 14:12?** _____

_____

Ahadi hii itatimizwa kwa njia gani? **Mdo 1:8**

_____

Yesu pia anasema kwamba tutatenda kazi kubwa alizozitenda na ***"kubwa kuliko hizi atazifanya"*** **(Yohana 14:12)**

- Aliwafufua wafu **(Mathayo 9:18)**
- Aliwaponya wagonjwa (**Luka 4:40)**
- Aliwabariki watu (**Mathayo 19:15)**

Yesu anatazamia wafuasi wake watende kama alivyotenda.

B. <u>Katika maisha ya kanisa la kwanza</u>.

1. Ubatizo ndani ya Roho Mtakatifu na kuachiliwa kwa karama za Roho Mtakatifu

Kama wanafunzi walivyowawekea waumini mikono, <u>waumini walibatizwa na Roho Mtakatifu na karama za Roho Mtakatifu ziliachiliwa au kuwekwa kwao.</u>

Ambacho wanafunzi walipokea kutoka kwa Bwana, waliweza kutoa kwa wengine kupitia kuwekea mikono.

(a) Mdo 8:14-18 Petro na Yohana waliwaendea waumini katika Samaria na wakawaombea **"*wapate kujazwa na Roho Mtakatifu".*** Ni nini kilifanyika **"*wakati walipoweka mikono yao juu yao"?* Aya 17:**

_____

_____

Lazima palikuwa na ishara ya kwamba kitu kimefanyika kwa njia ya kuwekea mikono kwa sababu Simioni **"*Alipoona ya kuwa watu wanapokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume"* aya 18.** Alitaka kununua ***"ili kila nitakaye muwekea mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu"* aya 19.**

(b) Soma **Mdo 19:4-6.** Ni nini kilifanyika wakati Paulo aliwatembelea wanafunzi kule Efeso? **aya 6**: _____

_____

(c) Sauli alipokea Roho Mtakatifu kwa njia gani? **Mdo 9:17**

_____

Ni karama gani iliwachiliwa hapa? **Aya 18**: _____

(d) 2 Timotheo 1:6 inaongea juu ya **kuachiliwa kwa karama ya mungu** iliyo ndani ya Timotheo kupitia kuwekewa mikono. Himizo la Paulo kwa Timotheo **"*chochea karama ya Mungu iliyo ndani yako"*** ni ukumbusho kwa waumini wote ya kwamba pasipo utendaji kazi wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu kupitia kudhihirishwa kwa karama za Roho Mtakatifu hatuwezi kuwa wahuduma wa injili ambao wanafaulu.
Katika **1 Timotheo 4:14,** Timotheo anakumbushwa tena asipuuze karama ambayo iko ndani yake ***"uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee"***

(e) Waefeso 5:18 tunakumbushwa daima kuendelea **"*kujazwa"*** na Roho mtakatifu

2. Kusimikwa na kutengwa kwa sababu ya huduma

a) Kwa majukumu Fulani - Kama kanisa la kwanza lilipoendelea kukua, ilionekana ni vyema kushiriki majukumu na kuwaweka watu waliochaguliwa wakfu kwa majukumu fulani ili mitume wawe huru kufanya kile kitu ambacho Mungu aliwaitia **(Mdo 6:2-6).**
Ni nini mitume walifanya katika **Mdo 6:6** kuwaweka watu hawa wakfu?

_____

_____

Tambua ya kwamba watu hawa tayari **"*wamejaa Roho Mtakatifu na hekima"*** (**aya 3**) *na* ***wamejaa imani na Roho Mtakatifu"*** **(aya 5).**
Matokeo yalikuwa yapi ya huku kutengwa kwa kuwekewa mikono?
Mdo 6:7 _____

_____

Paulo anapatiana onyo katika **1Timotheo 5:21-22** juu ya kuwachagua watu ***"kwa upendeleo"*** na kwa haraka kuwawekea mikono.

b) Kwa kuwekwa wakfu na kuachiliwa. (mwanzo wa huduma ya umishonari).
Mdo 13:2-3*:* ni maagizo yapi ambayo RohoMtakatifu aliagiza?_____

_____

Manabii na waalimu katika Antiokia waliitikia namna gani? _____

_____

Walikuwa **"*wamepelekwa na Roho Mtakatifu*" (aya 4); *"wakilihubiri neno la Mungu"* (aya 5); *"walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu"* (aya 9) *"wakafanya miujiza mikuu"* (aya 11) *"hivyo kwamba wengine wakaamini"* (aya 12).**

3. **Uponyaji.**
   Anania anamwekea Sauli mikono anapokea kuona**. (Mdo 9:17-18)**
   Paulo anamwekea baba yake Publio mikono kule Melita na akapona. **(Mdo 28:8-9).**

Wanafunzi walitii yale maagizo ya Yesu (Mariko 16:18), **"*Bwana akifanya kazi pamoja nao akilidhibitisha neno lake kwa miujiza iliyo wafuata"***

NI NANI ANAWEZA KUHUDUMU KUPITIA KUWEKEA MIKONO?

1) Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuachiliwa kwa karama za Roho Mtakatifu:

Mdo 8:17: _____

Mdo 9:17:_____

Mdo 19:6:_____

2Timotheo 1:6:_____

2) Kutengwa :

1Timotheo 4:14_____

Mdo 13:1_____

3) **Uponyaji:**

Mdo 9:17_____

Mariko 16:17,20: _____

Mdo 28:8*:* _____

Hebu tuombe sasa kwa ujazo waRoho Mtakatifu na kwa kuachiliwa kwa karama za Roho Mtakatifu kupitia kuwekewa mikono- ili kusudi la Mungu liweze kupitishwa kupitia watu wake kwa nguvu zake.

KUFUFULIWA WAFU

Kulingana na **Waebrania 6:1-2**, kufufuliwa wafu ni fundisho la msingi wa maisha ya mkristo. Paulo anasema, **"*Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngaliko katika dhambi"* 1Wakorintho 15:16-17.**
Kwa njia nyingine ni kwamba kufufuliwa wafu kumeunganishwa na kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristo na pasipokuwa na kufufuka, hapana uzima.

Kufufuka ni nini? Haswa, kuinua, kuamka; kuamka kutoka kifo.

Kuna vipengele vitatu muhimu ya fundisho la kufufuliwa wafu:

1. Kufufuliwa kwa Yesu Kristo
2. Kufufuliwa kiroho kwa waumini katika Yesu Kristo;
3. Hatima ya kufufuliwa kwa ***"wote walio makaburini"*** **(Yohana 5:28-29)**

KUFUFULIWA KWA YESU KRISTO

(Andika maandiko palipo na nafasi)
Mathayo 28:6:_____

_____

1Wakorintho 15:20: _____

_____

Matendo 2:24: _____

_____

Tunajua aje kuwa alifufuka?
Mdo 1:3:_____

_____

1Wakorintho 15:5-8: _____

_____

_____

_____

Alikuwa na mwili wa namna gani alipofufuka?

Yohana 2:19-22:_____

_____

_____

Luka 24:22-24: _____

_____

_____

Luka 24:36-40 _____

_____

_____

Yohana 20:27-28 _____

_____

_____

Unabii katika Agano la Kale kuhusu kufufuka kwa Kristo:
Zaburi 16:8-1: _____

_____

_____

Zaburi 68:18: _____

_____

_____

Isaya 53:10-12:_____

_____

_____

Maandiko yanazungumza kuhusu Mungu wa Ibrahimu, Isaaka na Yakobo. Yesu anasema: **"*Yeye sio Mungu wa waliokufa bali wa walio hai"* (Mathayo 22:31-32).**
Wanafunzi walimuona Eliya na Musa wakitokea pamoja na Yesu katika mlima. (**Mathayo 17:3)**
Maandiko yafuatayo katika Agano la Kale wazi inaonyesha maisha ya kufufuka. Andika aya hivi na utafakari maana yake.
2 Wafalme13:20-21 _____

_____

Mwanzo 22:5 _____

_____
Kwa wazi Ibrahimu alikuwa akitazamia maisha ya kufufuka, kwa maana Isaaka alikuwa mwana wa ahadi na kupitia yeye Ibrahimu alikuwa awe baba wa mataifa mengi ***(Mwanzo 17:19).***

Henoko katika **Mwanzo 5:24** na **Wabrania 11:5: _____**

_____

____ _____

Eliya **(2Wafalme 2:11)** na Musa **(Yuda 9**): _____

_____

_____

Ufufuo wa Yesu Kristo unatufundisha nini?

i. Yeye ni Mwana wa Mungu

Warumi 1:4 _____

_____

ii. Kifo kimeshindwa

Warumi 6:9_____

_____

iii. Yesu Kristo yuko juu ya wote wenye uhai

Mathayo 28:18_____

_____

Waefeso 1:20-23_____

_____

iv. Kuna mtu katika enzi ya mbinguni

Waebrania 10:12_____

_____

v. Waumini wanafanywa haki

Warumi 4:25*:*_____

_____

vi. Kuna chemichemi mpya ya uzima ya mwanadamu

1Petro 1:3_____

_____

vii. Hukumu ya milelel imehakikishiwa

Mdo 17:31*:*_____

_____

UFUFUO WA KIROHO WA WAUMINI

Waefeso 2:1, 5-6: _____

_____

Warumi 6:8: _____

_____

Wakolosai 2:13_____

_____

Wagalatia 2:19-20_____

_____

2Wakorintho 5:14-15_____

_____

Waefeso 1:15-23 inasema nini kuhusu nguvu za kufufua za Mungu katika maisha Yetu?

_____

Nguvu hizo ni zipi Katika **Waefeso 3:20**?_____

_____

Ufufuo wa Yesu una maana gani katika maisha ya muumini?

Yohana 5:25:_____

_____

Warumi 6:4-5: _____

_____

Wakolosai 2:12:_____

_____

Kuna uhakika upi wa ufufuo huu katika maisha ya muumini?

i. Nia ya imani inaimarishwa na inadumishwa

Warumi 6:11:_____

_____

ii. Maisha mapya yanadhihirika

Warumi 6:4:_____

_____

iii. Bwana mpya anatumikiwa

2Wakorintho 5:15:_____

_____

iv. Kusudi mpya ya maisha inakumbatiwa

Wakolosai 3:1-2_____

Katika **Wafilipi 3:10-12**, Paulo anaunganisha mitazamo mitatu ya fundisho la kufufuliwa wafu katika maombi yake ya ndani:

i. Ili nipate kumjua na nguvu za kufufuka kwake – nguvu hizi zinapatikana kwa waumini;
ii. Anatambua msingi wa uhakika wa kufufuka kwa Yesu na kupatikana kwa Nguvu za kufufuka kwake;
iii. Lengo lake ni kufufuka kwa wenye haki- ***"ili nipate kuifikia".***

KUFUFUKA KWA MWISHO KWA KILA MTU ALIYEKUFA

Wafu wote watafufuka toka kwa makaburi:
Yohana 3:28-29_____

_____

Mdo 24:15 _____

_____

Ufufuo utafanyika lini?
Yohana 6:39-40, 44, 54: _____

_____

Yohana 11:23-24:_____

_____

1Wakorintho 15:20-23: _____

_____

1Wathesalonike 4:16:_____

_____

1Wakorintho 15:51-52: _____

_____

Ufufuo wa wale wasio wa Kristo utafanyoka lini kwa kuja kwake?
Ufunuo20:11-15_____

_____

Ni nani afufuaye wafu?
1Wakorinto 6:14_____

_____

2 Wakorintho 1:9: _____

_____

2 Wakorintho 4:14: _____

_____

Yohana 6:39-40,44,54: _____

_____

_____

Tunapaswa kuhubiri kufufuliwa wafu
Mdo 4:2: _____

_____

Mdo 17:18_____

_____

Mdo 17:32: _____

_____

Mdo 23:6: _____

_____

Waumini watakuwa na miili inafanana aje?

i. **1 Wakorintho 15:38** _____

_____

ii. **1 Wakorintho 15:43**_____

_____

iii. **1 Wakorintho 15:44**_____

_____

iv. **1 Wakorintho 15:42, 50-53**_____

_____

v. 1 **Wakorintho 15:20 _____**

_____

1Wakorintho 15:49: _____

_____

Wafilipi 3:21: _____

_____

1 Yohana 3:2:_____

_____

Tumaini la kufufuliwa wafu linaadhirisha utendaji wetu
1Wakorintho 15:32-34 _____

_____

I Wakorintho 15:58: _____

_____

1Yohana 3:3 _____

_____

ILI NIMJUE YEYE, NA UWEZA WA KUFUFUKA KWAKE, NA USHIRIKA WA MATESO YAKE, NIKIFANANISHWA NA KUFA KWAKE ***Wafilipi 3:10***

HUKUMU YA MILELE

Kufahamu hali ya milele: kuishi milele katika ufalme wa mbinguni na Mungu;
au **kuishi milele kusimu – kutengana na Mungu milele.**

Maandiko yanatuambia kwamba kuna dhawabu kwa wenye haki mbinguni msingi wake ukiwa huduma zao katika utiifu kwa Bwana katika maisha yao.

Maandiko pia yanatuambia kwamba kuna adhabu kusimu msingi wake ukiwa vile mtu alimchukua Kristo na ndugu zake.

Yesu anaonya

- **Wanaoona na kusikia lakini hawatubu**

Mathayo 11:20-24*:* Watu katika mji huo waliona na kusikia nini?

_____

_____

- na wale ambao **wanasikia lakini hawatendi**

Mathayo 24:40-45: Ni nini ambacho watu hawa **hawakutenda?**

_____

_____

_____

Maana ya neno:

Kuhukumu = kutenga; kufanya tofauti kati; kufanya hukumu juu ya; kukadilia, kuwajibika; kujaribu; kuhukumu; kuweka katika kiasi.

Ni nani anahukumiwa?

Mara tu watu wanapokuja katika imani wanaondolewa katika hukumu na wanaletwa katika uzima.

Soma **Yohana 3:16-21** na uandike **aya.18**

_____

_____

"Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote <u>wasiomcha Mungu</u>, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao <u>wenye dhambi</u> wasiomcha Mungu wameyanena juu yake" **Yuda 15-15.**

Ni nani ambaye hatahukumiwa?

Yohana 5:24*:* _____

_____

Imani huelekeza kwa uhuru kutoka kwa hukumu, hivyo ni kuamua, na hii inaleta uzima badala ya kifo. **Warumi 8:1**_____

_____

_____

Kuelewa hukumu

Waumini

Waumini watahukumiwa kulingana na "***mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri aliyotenda, kwamba ni mema au mabaya".*** Maandiko yanasema, "***imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo"* (2Kor 5:10).**

"***Kwa hiyo, tena, ikiwa tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa, twajitahidi kumpendeza yeye"* (2Wakorintho 5:9*).*** Kama waumini tunahitaji kuishi maisha yetu, tukijua kwamba kuna uwajibikaji wa huduma zetu kama waumini.

Wasioamini

Wasioamini tayari wamehukumiwa kwa kukosa kumuamini Yesu Kristo. Biblia inaongea kuhusu hukumu kuu ya mwisho ambapo wafu wote watahukumiwa na Mungu. Yahana alisema, "***Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu zikafunguliwa"* Ufunuo 20:11-12**

Jawabu ni gani?

Wasioamini wote watapitia hukumu ya mwisho, lakini kitu cha muhimu ni kwamba tunapokuja kwa imani ndani ya Yesu, tunakombolewa kutoka kwa hukumu, kwa sababu Yesu alizichukua dhambi zetu msalabani. Ndiposa tunatakiwa kuihubiri injili. ***"Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"*** (**Warumi 3:23).** Wote wameasi sheria za Mungu. Adhabu ya kifo ni mauti (**Warumi 6:23**): kifo cha kiroho na cha kimwili ikielekeza kwa kifo cha kiroho milele. Tukimwamini Yesu Kristo na tukubali msamaha wa dhambi zetu kupitia sadaka yake msalabani, tunaokolewa kutoka kifo hadi uzima. Tunaokolewa kutoka kwa hukumu na hukumu tunayo hitaji.

2 Wakorintho 5:21: _____

_____

_____

Baadhi ya maandiko ambayo yanaeleza hukumu ya, na dhawabu ya wakristo

1. **Uzima wa milele: Mathayo 25:46:** _____

   _____

   [Nukuu **Yohana 3:16]**

2. **Toa hesabu**: **Warumi 14:12**: _____

_____

1 Wakorinto 4:5: _____

_____

_____

3. **Kazi ya kila mmoja: 1Kor 3:12-15 (**andika kwa mktasari)

_____

_____

_____

_____

4. **Mambo yaliyofanywa katika mwili: 2 Wakorintho 5:10**:

_____

_____

5. **Taji ya haki**: **2 Timotheo 4:8:**

_____

_____

Mbinguni kunafanana namna gani?

i. Mungu yuko mbiguni, **Matahayo 6:9:** _____

_____

Yeye hutazama kutoka mbinguni**, Zaburi 14:2:**_____

_____

ii. Ni enzi ya Mungu, **Isaya 66:1**

_____

_____

iii. Mbingu inatawala dunia , **Danieli 4:26** na **Mathayo 6:10**:_____

_____

_____

_____

iv. Uzima wa mbinguni ni wa milele, na Yesu alitoka Mbinguni, **Yohana 6:51:**

_____

_____

_____

v. Kuna dhawabu ambayo msingi wake ni tumaini la mbinguni kwetu **Wakolosai 1:5**

_____

vi. Mbinguni ni Pahali pa furaha, amani na haki katika Roho Mtakatifu, **Warumi 14:17**:

_____

_____

vii. Hakuna uchungu, machozi, kifo ama huzuni kwa maana Mungu yupo huko na anawatazama watu wake kikamilifu, **Ufunuo 21:3-4**

_____

_____

Ufalme wa Mungu *na* ***ufalme wa mbinguni*** *zote zinaongea kuhusu mbinguni. Kwa hivyo maandiko kuhusu ufalme wa Mbinguni na ufalme wa mungu inatusaidia kuelewa jinsi mbinguni kunafanana. Ni kusudi la Mungu mbingu ijulikane hapa duniani. Hii ndio injili ya ufalme na ujuzi wetu wa ufalme wa mbinguni unaanza kwa kuzaliwa upya.*

Warumi 14:17 *inaeleza ufalme wa Mungu hapa duniani. Ndio tutakayotambua katika kuja kwa Kristo: Mbingu duniani*
Ufunuo 21:3-4 *Inaelezea jinsi maisha yatakavyo kuwa hapa duniani wakati Mungu yupo kikamilifu na watu wake – mji mtakatifu umeshuka kutoka mbinguni.*

Mungu anahukumu kwa njia gani?

a) Kulingana na nuru ambayo watu wamepokea:
Warumi 2:12: _____

_____

Tafadhari soma: **Warumi 1:20, Mathayo 12:41-42.**

b) Kulingana na ukweli wa neno:
Warumi 2:1-2_____

_____

Tafadhari soma: **Yohana 12:47-48**_____

_____

c) Kulingana na mtendo:

1 Petro 1:17*:* _____

_____

Ufunuo 20:12-13: _____

_____

Inahusisha makusudi ya moyo:

Warumi 2:16: _____

_____

Tafadhari soma: **1wakorintho 4:5** na **Waebrania 4:12-13** na **1 Samweli 16:7.**

d) Bila kipendeleo – Mungu hana kipendeleo:

Warumi 2:11: _____

_____

Tafadhari soma: **Yakobo 3:17**, Hekima ya Mungu haina upendeleo.

e) Katika haki:

Soma **Zaburi 9:8**

Mdo 17:31: _____

_____

2 Timotheo 4:8: _____

_____

f) Kulingana na kutii kwetu kwa injili:

2 Wathesalonilke1:18:_____

_____

Kuzimu kukoje?

i. Adhabu ya milele, **Mathayo 25:46**: _____

_____

ii. Uharibifu wa milele kutoka kwa uwepo wa Bwana, **2 Wathesalonike1:8-9** na **Ufunuo 11:18:**_____

_____

_____

iii. Ziwa la moto, **Ufunuo 20:15** _____

_____

iv. Moto ambao hautazimika, funza wao hafi, **Mariko 9:43-48:**

_____

_____

_____

v. Mahali pa kuchanganikiwa, **Mithali 27:20** _____

_____

vi. Mahali pa kifo na uasi, **Zaburi 55:15, Zaburi 9:17** _____

_____

_____

vii. Mahali pa mateso, **Luka 16:23,** kwa miali **aya. 24**: _____

_____

_____

viii. Uzima wa uovu (Ubinafsi) ni mlango wa kusimu, **Luka 16:25**: _____

_____

ix. Mahali pa kutenganishwa na kilicho chema na cha kuleta faraja ya moyo, **Luka 16:26**:

_____

_____

x. Mahali pa huzuni, **Zaburi:18:5, 2Samweli 22:6** _____

_____

_____

xi. Upumbavu huelekeza kusimu, **Zaburi 9:18**: _____

_____

xii. Mahali pa hukumu ya milele, **Mathayo 23:33**: _____

_____

MAHALI PA WAFU

Panaitwa ***Sheol*** katika Agano la kale; na ***Hades*** katika Agano jipya. Maneno yote mawili yanawakilisha mahali pa wafu; eneo la roho zilizotoweka za wanadamu; pia eneo la roho za mapepo. Kabla ya Kristo kuja, kusimu ilihusisha 'wenye haki waliokufa walikuwa pale wakiongojea Yesu aje awakomboe kutoka mahali hapo na kuwaleta katika himaya ya mbinguni.'

Katika hadithi ya yule tajiri na Lazaro katika **Luka 16:19-31**, wenye haki waliokufa waliwekwa mahali salama katika kusimu, palipoitwa kifuani cha Ibrahimu. Wasio haki wako pahali pa mateso kutoka wakati ambapo nafsi zao zianaacha maisha haya. Tangu Yesu Kristo alikuja na akaondoa dhambi zetu kupitia msalaba, waliokufa katika imani wanaelekezwa mara moja katika uwepo wa Mungu, ***"kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana***" **2 Wakorintho 5:8.**

Katika kusimu, kabla ya msalaba kulikuwa na pahali pa wenye haki waliokufa, lakini palikuwa na pahali pa mateso, ambapo tunapajua kama ahera. Neno linalotumika katika Biblia la ahera ni neno *geenna*, linaloandikwa kwa kingereza *Gehenna.* Gehenna iliwakilisha pahali pa bonde la Hinnom, nje ya Yerusalemu ambapo takataka yote na uchafu wa mji zilikuwa zikitupwa na palikua pakichomwa daima na moshi yake inaendelea kuinuka. Hii ndio sehemu ya kusimu ambayo yule tajiri alijikuta akiteseka.

Hakuna mahali pa kungonjea paitwapo Purgatori katika mafumdisho ya wakatoriki wa Kirumi. **Waebrania 9:27** ***"Na kama vile watu wamewekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu".*** Wakati mtu anakufa, kihalisi mwili unakufa, na unarudi kwa udongo, lakini nasfi ya mwanadamu inaishi milele.

Hii ndio sababu imani katika Yesu Kristo ni ya muhimu sana na inatakikana, kwa maana njia ya kipekee ya uzima wa milele na Mungu ni katika imani ndani ya Yesu Kristo. Wale ambao wamekataa kumwamini Yesu Kristo na wale ambao wanakosa kuitii injili, **"*Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake"*** 2 **Wathesalonike 1:8-10.**

Dawa ya hukumu ni rehema!

Hatupaswi kuhukumu ila kwa maelekezo ya Mungu, kwa mfano, Paulo alihukumu uasherati katika **1 Wakorintho 5:3.** Tunawaonya watu kuhusu hukumu ambayo iko karibu, **Yakobo 5:8-9.**

Tunatakiwa kuhubiri rehema nyingi za Mungu za kuokoa na kusamehe! Rehema za Mungu ni kwamba yeye **"*hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba"* 2 Petro3:9.** Watu wanaweza kuokoka kwa kuja kwa ufahamu wa kweli **(1Timotheo2:4).** Tunaweza kuwafikia wengine na ushuhuda wa Yesu, kwanza kwa maombi na pili katika kuhubiri.

Warumi 11:33 *"**Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani".***

KUUFIKILIA UTIMILIFU

Waebrania 6:1 ***"Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu*** **[ukomavu, ukamilifu},… "**
Mara misingi imekwisha kuwekwa hebu tusonge mbele. Kuna mifano mingi ya ukomavu katika maandiko ikihusisha:

1. Mfano wa kanisa lililokomaa katika **Waefeso 4, huduma tano zikifanya kazi kikamilifu na mwili wote ukitenda kazi;**
2. Mwelekezo wa **maisha na tabia za ukomavu katika Warumi 12:9-21;**
3. Njia ya **kuhuduma karama za Roho pakiwa na upendo 1 Wakorintho 12-14;**
4. Muundo na tabia **ya mtu mpya katika Kristo katika Wakolosai 3:1-17;**

Katika somo hili tunachukuwa maandiko machache katika kitabu cha Waebrania kama hicho ndicho kifungu cha kwanza katiko mfululizo huu wa masomo.

Mwandishi wa Waebrania anahusika na wakristo hawajahitimu kutoka kwa maziwa ya neno la Mungu. Petro anayaita maziwa, "***neno la wokovu"*** **(1Petro 2:1 NASB*).*** Waebrania inanakili misingi sita ya imani kama maziwa ya neno na anaita ***"nyama ya neno", "neno la haki"*** **(Waebrania 5:12-14).** Mtu aliyekomaa ni mtu **"*aliye na ujuzi katika neno la haki****"*** na anaweza ***"kubabanua mema na mabaya***" kupitia kuzoea (utendaji) akili za kiroho. Njia ya ukomavu ni kwa njia ya mazoea. Hakuna njia ya mkato. Ni lazima tupate ujuzi ili tukue.

Paulo anasena, "*Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya wanayoitawala dunia hii, wanaobatilika; bali twanena hekima ya Mungu katika siri…"* (**1 Wakorintho 2:6-7).** Hekima hii hufunuliwa na Roho **(aya 10). Hekima ya Mungu huja kupitia kwa neno. Tumeitwa tujifundishe neno la Mungu.**

*Mwandishi wa Waebrania anasema kwamba tutaenenda katika ukomavu Mungu akitujalia; "****haya tutafanya Mungu akitujalia"*** **(6:3**). Mungu ataturuhusu tu kwenda katika neno lake kwa undani kama tumetii katika kuiweka misingi sawasawa. Kwa njia nyingine ni bure kwetu kutafuta kuingia sana katika neno la Mungu kama hatujazamishwa kwa maji kwa kubatizwa kikamilifu kulingana na maandiko, kupitia kuwekewa mikono. Sisi sote pengine tunaweza kukubali tulifunzwa vibaya msingi wa kufufuliwa wafu na hukumu ya milele. Hebu Mungu atufunulie ukweli huu na arejeshe uhakika wake katika kanisa lake siku zetu.

TARAJIA KUWAONA WAFU WAKIFUFUKA!
TARAJIA KUONA HUKUMU YA MUNGU KANISANI
KAMA ILIVYO KATIKA MATENDO 5

1. KUWA NA UWEZA WA KUFUNDISHA

"***Iwapasapo kuwa waalimu"***

Katika **1 Peter 4:7-18,** mtume anatoa mwelekeo wa huduma na mateso kama mkristo aliyekomaa. ***"Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; na mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu;*** **(aya 11)**

Katika **Wakolosai 3:17,** Paulo anasema **"*Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye"*** na katika **4:6** ***"Maneno yenu yawe na neema sikuzote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kujibu kila mtu"***

Mojawapo ya hitimu ya mzee ni ***"kuwa na uweza wa kufundisha"*** **(1Timotheo 3:2)** Mungu anataka kumpa kila mmoja **"*fundisho"*** kushiriki katika mkutano (**I Wakorintho 14:26).**

2. TUNAFUNDISHA NINI?

a) Tunafundisha mwana wa Mungu ni nani? **(Waebrania 1)**
Kuna nukuu nyingi za Agano la Kale katika kitabu cha Waebrania. Kwa kusoma nukuu hizi tunasoma na kufahamu maandiko ya Agano la kale, tukimwona Yesu katika hayo. Katika **Luka 24:44-45**, Yesu alifungua ufahamu wao wa Masihi katika maandiko ya Agano la kale. Je macho yako yamefumbuka? Unaweza kuwaonyesha wengine Yesu katika maandiko ya Agano la kale?

b) Fundisha kuhusu masalaba na mazao mengi ya msalaba, uhakika wa Mwana wa Mungu akiwa mtu wa mateso ya kifo; kushindwa kwa shetani, muundo halisi ya maisha yaYesu **(Waebrania 2)**

c) Fundisha habari ya uaminifu wa Yesu, na kutokuaminika kwa kanisa la Musa – shida ya kutoamini; jinsi ilivyo muhimu kulishika neno la Mungu leo **(Waebrania 3)**

d) Fundisha *"habari ya raha ya Mungu"* na nguvu za neno la Mungu la kutuleta ndani ya raha yake **Waebrania** (**4:1-12).** Je hii ni sabato ya mapumzika?. Maagizo ya **"*weka sabato"*** yamaanisha nini? Biblia inafundisha ***"raha ya Mungu"*** kutoka ***Mwanzo 2:2-3.*** Mungu alimaliza kazi yake ya uumbaji na akapumzika; siku ya saba ilikuwa kamilifu, siku ya milele bila asubuhi wala jioni. Sabato ambayo Yoshua alisema ilikuwa zaidi ya sabato ya kawaida; alikuwa akitazamia sabato ya Mungu.

e) Fundisha kuhusu kuhani mkuu, **"*mpangilio wa Melkizedeki"*** – mtume anashugulika sana ya kuwa wakristo wa kiebrania wanajuwa machache kuhusu melkizedeki, nasi tunajua kidogo! (**Waebrania 5 na 7).** Kutajwa kwingine kwa Melkizedeki ni katika **Mwanzo 14 na Zaburi 110.** Hata hivyo kuna mafundisho mengine ya kote kote katika maandiko kuhusu Mfalme/Kuhani na ***"Ukuhani wa Kifalme"*** **1Petro 2:9.**

Pengine maswali mawili ambayo ninaulizwa sana kama mwalimu ni: ni dhambi gani ambayo haiwezi kusamehewa? Na Melkizedeki ni nani? Unaweza kujibu swali la pili?

f) Hakikisha misingi imefundishwa vyema; onya kwamba tunaweza enda mbali sana tukitoka kwa wokovu - hakuna toba ingine kwa wale wako kama Esau (maandiko yanatufundisha nini kuhusu dhambi ambayo haiwezi kusamehewa?): lakini kuna tumaini la kweli; ni kwa imani na saburi kwamba tunarithi ahadi **(Waebrania 6).**

g) Fundisha kuhusu ukuhani – ukuhani mpya na bora; tazama zaidi kumhusu Melkizedeki- ametajwa mara ya kwanza katika **Mwanzo 14** na kutajwa katika **Zaburi 110**. Pia kuna fundisho katika **Waebrania 7**. Soma kwa makini pasina kuongezea wala kutoa ndani yake. Kisha unaweza kuwajibu watu moja kwa moja kutoka kwa maandiko **(Waebrania 7)**

h) Fundisha kuhusu huduma mpya za kikuhani: kuna muundo wa ibada! na Agano jipya; liko jipya namna gani? (**Waebrania 8).** Tunamuabudu Baba kwa njia gani **"*Katika Roho na kweli"***

i) Tunaingia aje katika patakatifu? Pako wapi? Madhabahu ya musa ni ya muhimu kwa jinsi gani? aya ***5, "Basi hutuna nafasi sasa kuelezea habari ya vitu hivi kimoja kimoja"***, lakini aya nyingi katika **Kutoka** zimetolewa kwa Hema; mara nane katika **kutoka 40**, inasema Musa akafanya kama vile BWANA alimuagiza **(Waebrania 9).**

Chukua **Waebrania 9:1-5** kama kielekezo na ujifundishe kuhusu Hema ya Musa. Damu ya Kristo iko wapi sasa? biblia inafundisha nini kuhusu damu ya Kristo?

j) Ni kwa nini Mungu anataka sadaka ya damu? Ni kwa njia gani ambapo sadaka ilionyesha Yesu katika sheria? – fundisha kuhusu utimilifu – jinsi Yesu alikuja kutimiza na kukomesha, onya dhidi ya dhambi; wenye haki wataishi kwa imani (**Waebrania 10)**

k) **Waebrania 11**ni kuhusu imani: kuna mengi sana katika sura hii. Unajua nini kuhusu waume na wake wa imani katika Agano la Kale? Unajua kufanya somo la tabia ya mtu na kufundisha ujumbe unaohusiana kutoka hapo?

l) **Waebrania 12** inatusaidia kumtazama Yesu, ili tuweze kushugulikia majaribio (urudi/ nidhamu); Nyumbani mwa muumini kunadhihirishwa: Sayuni! Unajua Sayuni? Huwa tunakwea kwenye mlima wa Mungu kwa njia gani?

m) Utamatisho katika **Waebrania 13** ni maelekezo yenye utajiri kuhusu kuishi na dhabihu za Rohoni za wakristo: sifa!

Kila eneo laweza kugawanywa hata zaidi na mafundisho ya kina kutolewa katika kila sehemu. Kitabu cha Waebrania kinakubali na kinahitaji maarifa ya ndani na ufahamu wa Agano la Kale. Hekima hii ni ya wale waliokomaa! Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi **"*Ukitumia kwa halali neno la kweli"* 2 Timotheo 2:15.**

"Walakini mwisho wa agizo hilo ni

Upendo utokao katika moyo safi

Na dhamiri njema,

na imani isiyo na unafiki"

(1Timotheo 1:5)